

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA**

IMEIDHINISHWA KWA KIWANGO CHA ISO 9001:2015



## TAARIFA KWA UMMA

### PROGRAMU YA USHIRIKA YA ROK-KAU 2026 KUHUSU SERA ZA KIMATAIFA ZA USAFIRI WA ANGA -KOREA

Mamlaka inapenda kuwataarifu watumishi wa umma na watumishi wa sekta binafsi wanaofanya kazi katika sekta ya usafiri wa anga kuhusu fursa ya kuomba kujiunga katika Programu ya Ushirika ya ROK-KAU 2026 kuhusu Sera za Kimataifa za Usafiri wa Anga (Korea Fellowship Programme on Global Aviation Policy), ambayo ni programu ya mafunzo ya uzamili ya kimataifa iliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha Anga cha Korea (Korea Aerospace University) kwa ushirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Korea.

**Programu hii itaanza mwezi Agosti 2026 na kukamilika mwezi Desemba 2027, ambapo washiriki watatunukiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Sera za Usafiri wa Anga (Master of Science in Aviation Policy).** Programu inalenga kujenga na kuimarisha uwezo wa wataalamu wa sekta ya usafiri wa anga kwa kuwapatia elimu ya juu na ujuzi wa kitaalamu katika maeneo ya sera za usafiri wa anga, usimamizi wa sekta ya anga na uendeshaji wa viwanja vya ndege katika ngazi ya kimataifa.

Mafunzo yataendeshwa kwa lugha ya Kiingereza, hivyo waombaji wanatakiwa kuwa na ufasaha wa lugha hiyo unaowawezesha kushiriki kikamilifu katika masomo na shughuli zote za programu bila kuhitaji huduma za tafsiri. Aidha, programu inatoa ufadhili kamili unaojumuishwa ada za masomo, tiketi za ndege za kwenda na kurudi, malazi katika mabweni ya chuo, posho ya kujikimu pamoja na bima ya afya.

**Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe Juni 28, 2026.**

**Vigezo:** Watumishi wa umma na sekta binafsi wenye vigezo wanahimizwa kuwasilisha maombi yao kwa kuzingatia masharti, taratibu na muda wa maombi kama ilivyoainishwa katika taarifa kamili ya programu.

Kwa maelezo zaidi kuhusu programu na utaratibu wa maombi, tembelea tovuti: [kau.ac.kr](http://kau.ac.kr)

Imetolewa tarehe **Juni 11, 2026.**

---

Dkt. Jabiri K. Bakari  
**MKURUGENZI MKUU**